JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAISI-TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA BUMBULI

SHULE YA SEKONDARI MBELEI,
S.L.P 109,
SONI.
14/05/2018.

NAMBA ZA SIMU:
Mkuu Wa Shule: 0784524029 / 0766805826.
Makamu Mkuu Wa Shule: 0714356735 / 0767356735.

Kumb: MBLS/JI/V1/005.

YAH: **FOMU YA MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MBELEI, HALMASHAURI YA WILAYA YA BUMBULI MWAKA 2018.**

MZAZI/MLEZI WA……..

1.0. KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO 2018/2019.

Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha tano (V) katika shule hii mwaka 2017-2018.Shule ya sekondari Mbelei ipo umbali wa kilometa 8.5 Km kutoka Mji mdogo wa SONI.Usafiri wa kutoka Soni hadi shuleni,ni Shilingi 4000/= hadi 5000/=Kutokea Dar es Salaam na Arusha, panda gari inayoelekea BUMBULI shuka kituo kinaitwa MBELEI na hapo utapata PIKIPIKI mpaka shule. Kwa wale wanaotoka maeneo mengine, panda gari inayoelekea LUSHOTO, shuka kituo kinaitwa SONI, hapo utapata PIKIPIKI itakuleta mpaka shuleni.

Pia kama gari uliyopanda haiendi kati ya sehemu hizo mbili yaani aidha BUMBULI au LUSHOTO ila linapita barabara ya TANGA-ARUSHA, shuka MOMBO. Hapo utapata gari za kwenda LUSHOTO au BUMBULI halafu fuata maelekezo ya kushuka SONI au MBELEI.

2.0. MAAGIZO MUHIMU YAKUZINGATIA.

2.1. **Sare ya Shule.**

(a) Sare ya shule hii ni,Shati nyeupe ya mikono mirefu,Sketi ya rangi ya Kijani Kibichi (Mshono Rinda box),Kizibao cha rangi ya Sketi,Sweta la Kijani Kibichi.Na Tai fupi (necktie) ya rangiMya Kijani Kibichi.Viatu vyeusi vya kamba na Soksinyeupe.

(b) Hijabu,Suruali ya rangi ya kijani kibichi,nusu kanzu nyeupe na ushungi mweupe.Sweta la kijani, viatu vyeupe vya kamba na soksi nyeupe.

(c) Sare za michezo ni track suti ya rangi ya bendera ya taifa na raba rangi yeyote.

(d) Shamba dress (gauni) la rangi ya kijani.

3.0. A: MICHANGO YA SHULE.

- Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi 70,000/= kwa mwanafunzi.Unaweza kulipa kiasi cha shilingi 35,000/= kwa muhula.
- Shilingi 15,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani.
- Shilingi 20,000/= kwa ajili ya taaluma,(Ilipwe mwanzo wa muhula)
- Shilingi 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho cha mwanafunzi.
- Shilingi 30,000/= kwa ajili ya kuwalipa wapishi,walinzi na vibarua wengine.
- Shilingi 2,000/= nembo ya shule.
- Shilingi 5,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza na Bima ya Afya

- Ths.5, 000/= (Wanafunzi washauriwe kujiunga na Mfuko wa Bima ya Afya CHF kikaya).
- Shilingi 5,000/= fedha ya tahadhari (haitarejeshwa)

Fedha hizo zilipwe katika akaunti ya shule Na:**41603500107**, Jina la Akaunti Ni; **Mbelei Sekondari** katika Benki ya **NMB** au apeleke kwa **Mhasibu wa Shule** kama hakuna benki jirani.
NB; **T-Shirt** itapatikana shuleni kwa gharama ya shilingi 15,000/=.

JUMLA KUU KWA MWAKA NI TSHS: 173,000/= Tu.

B: MAHITAJI MENGINE.

- Godoro moja(1) {Futi sita kwa mbili na nusu}
- Mashuka mawili ya rangi ya bluu au pinki.
- Blanketi moja (1)
- Mto mmoja (1)
- Sahani,bakuli, kijiko na ndoo mbili.
- Ream moja ya A4.
- Madaftari saba (7) ya Quire 3 au 4.
- Mkebe mmoja (1)
- Chandarua
- Fyekeo au Jembe
- Kamusi ya Kiingereza moja (1)
- Picha pasipoti saizi mbili (2)
- Scientific calculator.
- Vitabu vya masomo tahasusi husika

4.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE:
Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Namba 25 ya miaka 1978.Aidha inazingatia miongozo yoteinayotolewa na wizara yenye dhamana na elimu nchini.Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayoyatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yako mara baada ya kuripoti shuleni.
(a) Heshima kwa viongozi,wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule.
(c) Kuhudhuria masomo (darasani) kila siku.
(d) Kutimiza kwa makini maandalizi ya jioni. (Preparation).
(e) Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
(f) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako hapa shuleni.
(g) Kutunza usafi wa mwili na mazingira kwa ujumla.
(h) Kuvaa sare ya shule wakati wote utakapotakiwa.
(i) Kuzingatia muda na ratiba ya shule wakati wote.

5.0. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA UKAFUKUZWA SHULE.
(a) Wizi shuleni.
(b) Uasherati,ushoga na ubakaji.
(c) Ulevi na utumiaji wa madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa bangi,mirungi,kubeli na sigara.

(d) Kupigana au kupiga.
(e) Kuharibu kwa makusudi mali ya shule na mali za wengine.
(f) Kudharau bendera ya shule(Taifa).
(g) Kuoa au kuolewa.
(h) Kupata mimba au kuharibu mimba ndani na nje ya shule.
(i) Kugoma,kuchochea na kuongoza mgomo na kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
(j) Kukataa adhabu kwa makusudi.
(k) Kuwa na simu ya mkononi shuleni.

6.0. MAMBO MENGINE MUHIMU.

(a) Medical examination form ambayo imejazwa na mganga mkuu wa hospitali ya wilaya.Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
(b) Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki kwenye migomo,fujo na makosa ya jinai.
(c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria za shule, kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa shuleni.
(d)Result slip original.

SOMA KWA MAKINI MAELEKEZO HAYA NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU.

KARIBU SANA

…….....
MKUU WA SHULE

The United Republic of Tanzania
PO-Regional Administration and Local Government

MBELEI HIGH SECONDARY SCHOOL,
S.L.P 109,
SONI.
14/05/2018.

Ref: MBLS/AD/A-L/004
To The Medical Officer
……
……
……

REF: STUDENT'S MEDICAL EXAMINATION FORM.
Please, examine the Pupil in respect to these areas and any other area (s) that is necessary to examine.

……
Head Master

Full name ……
Age: ……. Sex……
Blood count (Red and White) …….
Stool examination …….
Urine Analysis ……..
T.B Test ……
Seeing ……..
Hearing ……..
Blood pressure ……..
Asthma ……

ADDITIONAL INFORMATION: e.g. Physical defects or impairment (s) infections, chronic or family diseases e.t.c
……
……
Do you therefore recommend this pupil to pursue studies at this school?
……
……. ……. ……. ……...

Name	**Signature**	**Date**	**Official Stamp**
……	**…….**	**……..**	**……**

OFISI YA RAISI
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA BUMBULI

SHULE YA SEKONDARI MBELEI,
S.L.P 109,
SONI.
14/05/2018.

FOMU YA KUKUBALI NAFASI ALIYOPEWA.

SEHEMU A: Habari za Mwanafunzi.

1. Jina kamili .....
2. Tarehe ya kuzaliwa .....
3. Wilaya alipozaliwa.....Kijiji.....
4. Kukubali nafasi (ijazwe na mwanafunzi)

Mimi ..... nimeona maagizo yote ya kujiunga na Shule ya Sekondari Mbelei na ninakubali kutimiza masharti yote ya shule ikiwa ni pamoja na uletaji wa vifaa vinavyohitajoka na kutii kanuni zote za shule. Nitakapokuwa shuleni Mbelei nitajitahidi kadri ya uwezo wangu kuzingatia yote ambayo wanafunzi wanatakiwa kutimiza katika suala zimala kupata Elimu ya kujitegemea.

Sahihi ya Mwanafunzi ..... Tarehe.....

SEHEMU B: Habari za Mzazi/Mlezi (Ijazwe na Mzazi/Mlezi)

1. Jina kamili.....
2. Yeye ni Mzazi/Mlezi.....
3. Kazi yake .....
4. Anuani ya Mzazi/Mlezi

.....

5. Namba TATU za simu ikiwemo ya Mzazi/Mlezi na ndugu wa karibu

i. .....
ii. .....
iii. .....

UTHIBITISHO

Mimi Mzazi/Mlezi wa ..... nimehakikisha kwamba maagizo yote yameeleweka na mtoto amejaza kikamilifu sehemu A.

.....
Mkuu Wa Shule